



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb Na.BDC/4/32/VOL.II/30

30/09/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo amepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hiyo, anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi 03 kama inavyoonekana hapa chini:-

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II-(NAFASI 02) TGS B.

SIFA ZA MWOMBAJI.

- Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
- Awe na cheti cha Astashahada (Technician Certificate- NTA LEVEL 5) cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika moja wapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

MAJUKUMU YA KAZI.

- Kutafuta Kumbukumbu/ Nyaraka/Mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- Kuthibiti upokeaji, uandikishaji wa Kumbukumbu / Nyaraka.
- Kuchambua, Kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/ Nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka / kupanga kumbukumbu, nyaraka katika reki(file racks/cabinets) katika masjala / vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka Kumbukumbu (barua, nyaraka nk) katika mafaili.
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/ nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

2. DEREVA DARAJA LA II – (NAFASI 01) TGS B.

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Kuajiriwa mwenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- **Waombaji wenye Cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.**


MAJUKUMU YA KAZI:-

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI.

1. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
3. Mwombaji aambatanishe Nakala ya Kitambulisho cha Uraia au Namba ya Kitambulisho hicho kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
4. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi(CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa.
5. Picha moja Passport size iandikwe jina kwa nyuma.
6. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results havitakubalika**).
7. Waombaji kazi ambayo tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **wasiombe kazi** na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
8. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya posta kabla ya tarehe **14/10/2021** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 70,
BIHARAMULO.


Dkt. Sospeter Budeba Mashamba
Kaimu: **MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BIHARAMULO

Nakala:- Ubao wa Matangazo,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 299
KAGERA.

Ubao wa Matangazo,
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 70,
BIHARAMULO.